

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA



Kumb.Na.BDC/C.30/17/72

11 Mei, 2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega anapenda kuwatangazia wakazi wote wa Wilaya ya Busega wenye sifa kujaza nafasi kumi na saba (17) za kazi za watoza ushuru katika maeneo yenye shughuli mbalimbali za biashara za mazao ya Uvuvi ambayo ni Kata ya Lamadi, Kalemela, Kabita, Nyashimo, Mwamanyili na Kiloleli. Kazi hii itakuwa ni ya Mkataba wa miezi mitatu na malipo yatalipwa kulingana na makubaliano kati ya Mwajiri na Mwajiriwa kwa kuzingatia fedha itakayokusanywa.

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe ni Raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na umri usiozidi miaka 45
- Awe na Elimu ya Kidato cha nne na Kuendelea
- Awe na uwezo wa kusikia, Kusoma na Kuandika
- Awe na uwezo wa kutumia simu janja (Smartphone)
- Awe na uzoefu katika masuala ya kukusanya ushuru
- Awe mwadilifu na mwaminifu na awe hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai.
- Awe ni mkazi wa Wilaya ya Busega hususani Kata husika.

Sanduku la Posta 157, Busega; Simiyu; simu-+255 (028) 2981193, Nukushi- +255 (028)2981194

Barua pepe: ded@busegadc.go.tz na Tovuti: www.busegadc.go.tz

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE.

- Waombaji wote wawe na wadhamini 02 walio na mali zisizohamishika.
- Waombaji wote wapitishie maombi yao kwa Mtendaji wa Kijiji/Kata.
- Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo binafsi (CV), nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- Picha moja Passport Size iandikwe jina kwa nyuma.
- Maombi yote yawe na namba ya simu na anuani halisi ya makazi

Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya kiingereza au Kiswahili na yatumwe kwa njia ya Posta au yawasilishwe kwa njia ya mkono Masjala-Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kabla ya tarehe **20/05/2021** kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P. 157,
BUSEGA.



Anderson Njiginya Kabuko,
Mkurugenzi Mtendaji,
HALMASHAURI YA WILAYA BUSEGA.

**MKURUGENZI MTENDAJI
H/ WILAYA YA BUSEGA**

Sanduku la Posta 157, Busega; Simiyu; simu-+255 (028) 2981193, Nukushi- +255 (028)2981194
Barua pepe: ded@busegadc.go.tz na Tovuti: www.busegadc.go.tz